



UNIVERSITY JOURNAL

ISSN: 2507-7864

EDITORIAL BOARD

Prof. Yunis Abdille MUSA

Chief Editorial Board

Prof. Fowzi Mohamed Barrow

Editor

Prof. Msafiri Mshewa

Prof. Mohamed Ali El-Kamil

Mr. Burhan Hatinbu muhuzi

Mr. Mohamed Haji Ali

Mrs. Mwanatumu Ali Hassan

Advisor Board

Prof. Amran Mohamed Rasli

(Chairman) SUMAIT University

Prof. Hamed Rashid Hikmany

SUMAIT University

Prof. Mustafa Adam Rushash

Zanzibar University

Prof. Said Ahmed Moh'd.

The State University of Zanzibar

Prof. Mohammed Al sheikh

The State University of Zanzibar

Dr. Miraji Ukuti Ussi

Commission for tourism, Zanzibar

Dr. Nassor Hamad Bakari

SUMAIT University

Dr. Mohamed Saleh Abdala

SUMAIT University

The Chief Editor,

SUMAIT University Journal of Scientific Studies,

P.O. Box 1933,

Zanzibar, Tanzania

Ph. +255-24-223-9396

E-mail: sumaitcrpc@gmail.com

Website: <http://www.sumait.ac.tz>

Annual Subscription: USD 5 (2 issues) for institutions, And USD 40 (2 issues) for individuals

ISSUE NO:5 DECEMBER 2018

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk♥

Abstract

This article presents some of the important elements of form and content in the plays of Mbaya **Wetu** (2014) written by Ken Walibora and **Amezidi** (1918) authored by Said Ahmed Mohamed. The aim of this article is to identify different artistic aspects of form used in their literary works based on the Effect and Intertextuality Theory. The article compares aspects of form such as structure and style. The structural aspects dealt with are character; plot and setting while in style the article deals with figurative language and other artistic method such as intertextual method, symbols and images. The article also presents the aspects which these writers share and differ from one another. The article establishes that, although the writers have used similar aspects, the difference between them exists. The difference has been caused by the types of plays, theory used, style, content and cultural environment surrounding the writers. This article is important in the field of comparative literature in which students will be helped to develop skills and understand how to compare literary works.

Ikisiri

Makala hii inachunguza baadhi ya vipengele vya fani katika tamthilia ya Mbaya Wetu (2014) ya Ken Walibora na Amezidi (1998) ya Said Ahmed Mohamed. Lengo hasa ni kubainisha vipengele tafauti vya kisanaa walivyotumia katika kubuni kazi zao. Makala hii imetumia nadharia ya athari na mwingilianomatini. Makala imezingatia ulinganishi wa vipengele vya fani kama vile, muundo na mtindo. Vipengele vya kimuundo vilivyoshughulikiwa ni wahusika, msuko na mandhari, na katika mtindo tumezingatia matumizi ya lugha na mbinu mbalimbali za kisanaa ikiwemo, mwingilianomatini, lugha ya picha na Ishara pamoja na kuchunguza namna ambavyo waandishi hawa walivyofanana ama kutafautiana. Makala imeonesha kuwa, ingawa waandishi wameweza kufanana ama kutumia vipengele vilivyo sawa lakini ipo tafauti kati yao. Hali imetokana na aina ya tamthilia, mkabala

♥ Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Luqhawiya, Choo Kikuu cha Abdulraman Al- Sumait, Zanzibar

aliotumia mwandishi, mtindo wa mwandishi, maudhui au mazingira ya utamaduni wa mwandishi husika. Makala hii ni muhimu katika uga huu wa fasihi linganishi kwa sababu itasaidia kuongeza ujuzi kwa wasomi katika taaluma hii na kuona namna kazi za fasihi zinavyoweza kulinganishwa.

Utangulizi

Fasihi Linganishi ni taaluma mpya katika uwanja wa fasihi za Kiafrika. Katika masomo ya elimu duniani, Fasihi Linganishi ni somo ambalo halina historia ndefu. Dhana ya Fasihi Linganishi inatokana na maneno ya Kifaransa “la Literature Comperee” yenye maana ya Comparative Literature katika lugha ya Kiingereza na kutafsiriwa Fasihi Linganishi kwa Lugha ya Kiswahili. Somo hili lilianza katika karne ya 19 huko Ufaransa, kisha likashika kasi na kuenea Ulaya na baadaye Marekani. Kwa hivi sasa taaluma hii imeenezwa katika nchi nyingi zikiwemo za Afrika Mshariki ambako hutumika katika fasihi ya Kiswahili.

Kulingana Mutembe (2016) katika dibaji yake ya Misingi ya Fasihi linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi na Jilala (2016), anafafanua kuwa, taaluma hii inajihusisha na ulinganishaji wa kazi za fasihi kwa lengo la kuchunguza jinsi kazi hizo za fasihi zinavyofanana na kuhusiana au kutafautiana katika vipengele vya fani na maudhui. Taaluma hii husaidia kugundua mambo tafauti yanayohusu jamii iliyoandikiwa pamoja na kuona tafauti za ubunifu wa mwandishi mmoja na mwengine na utamaduni wa jamii moja na nyengine. Kwa maana hiyo, kazi za fasihi duniani zinaweza kufanana ama kutafautiana kutokana na nguvu maalum ya kimaumbile inaowaunganisha wanadamu wote kutokana na mazingira ya jamii, mahitaji ya kimwili na kijamii. Hivyo, ulinganishaji huo wa vipengele vya fani vilivyoshughulikiwa katika makala hii, ni mfano muafaka wa kuelewa vyema taaluma hii na kuona tafauti iliyopo kati ya waaandishi hawa.

Maana ya Fasihi Linganishi

Boldor (2003) akimrejelea Compbell (1926), anaeleza kuwa, Fasihi Linganishi ni taaluma inayochunguza uhusiano uliopo baina ya fasihi mbili au zaidi, nje ya mipaka ya kitaifa kwa njia ya kulinganisha mfanano na msigano.

Guyard (1951) kama alivyonyukuliwa na Weisstein (1973) anasema kuwa, Fasihi Linganishi ni tawi la historia ya fasihi. Ni somo la mahusiano, mapatano na maelewano ya kitaifa ya kazi na hata maisha ya waandishi wanayotoka, katika jamii

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

zenye fasihi tafauti. Ameonesha mfano wa waandishi wanaotafautiana baina yao, kama, Byronna Pushkin, Goethe na Carllyle, Waltercott na Alfred de Vignyna. Maelezo haya yamefafanuliwa na Jilaa (2016) anayeeleza kuwa, taaluma hii inashughulikia mahusiano baina ya jamii moja na nyengine na kuonesha maingiliano ya jamii kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hapa mwanafasihi linganishi anaweza kujiuliza maswali: Jamii hizi zinakutana wapi? Mambo gani yanadhihirisha kuingiliana na kufanana kwa kazi ya fasihi?

Van Tieghem (1931) Kama alivyonyukuliwa na Wellek (1988), anaifasili fasihi linganishi kuwa ni somo linalojishughulisha na uhusiano wa vitu viwili vinaweza kuwa kazi ya mtu binafsi, waandishi au kundi la waandishi na binaadamu au fasihi kwa ujumla. Kwa upande wa Wellek (1988) anaona Fasihi Linganishi kuwa ni taaluma ya fasihi inayozingatia fasihi iliyo nje ya mpaka wa nchi moja, inayompa mtu fursa ya kujifunza uhusiano baina ya fasihi kwa upande mmoja na eneo au maarifa mengine kama sanaa, falsafa, historia ya sanaa za jamii, sayansi, dini na kadhalika. Pia, anaieleza Kwa ufupi kuwa, ni ulinganishi wa fasihi na fasihi nyengine na ulinganishi wa fasihi na mzunguuko wa maelezo ya binadamu.

Bassnet (1993) anaiona fasihi linganishi kuwa ni taaluma ya usomaji matini za tamaduni tafauti ili kubaini mazingira zinapokutana na zinapoachana. Vilevile, Wellek na Warren (1996) wanaeleza kuwa, fasihi linganishi ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi hata wanasayansi kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni.

Fasihi linganishi hushughulikia ulinganishi wa fasihi na kazi nyengine za kisanii. Kwa mfano, mlinganishaji anaweza kulinganisha au kuchunguza uhusiano uliopo kati ya filamu na fasihi, kazi za sanaa za uchoraji, uchongaji na uhunzi na fasihi. Mathalani, kwa kutumia fasihi linganishi mhakiki anaweza kulinganisha kazi za Said Ahmed Mohamed za (1980) na (2000), au Shaaban Robert katika vipindi tafauti katika uandishi wake n.k.

Kutokana na maelezo na fasili zilizotolewa hapo juu na wataalamu mbalimbali kuhusu fasihi linganishi, inaonesha kuwa, wataalamu hao hawatafutiani sana katika mielekeo na mitazamo yao juu ya Fasihi Linganishi. Wanakubaliana kuwa Fasihi Linganishi ni taaluma inayoshughulikia ulinganishaji wa kazi za fasihi. Ni taaluma inayoshughulikia tafauti au kufanana Kwa fasihi ya makundi mawili au zaidi kiisimu, kiutamaduni, kihistoria, kiitikadi, kiuchumi, kijamii, kitaifa na kimataifa. Pia, fasihi

linganishi hulinganisha fasihi ya lugha moja, ikiwa fasihi hiyo itatokana na jamii tafauti ndani ya lugha moja.

Maeneo ya Ulinganishaji

Katika taaluma ya fasihi linganishi, mhakiki anaweza kuchunguza kufanana na kutafautiana kwa vipengele kama matumizi ya lugha, maudhui, falsafa za waandishi na utamaduni. Mhakiki anaweza pia kulinganisha kazi za fasihi za kipindi fulani cha kihistoria na kipindi chengine cha historia. Mathalani, kazi zilizoandikwa kabla ya uhuru na zilizoandikwa baada ya uhuru; kipindi cha siasa ya Ujamaa na Kujitegemea au Azimio la Arusha nchini Tanzania; mfumo wa uchumi huria; mfumo wa itikadi ya chama kimoja na wakati wa vyama vingi kisiasa. Ulinganishi huu unawawezesha wahakiki kubainisha tafauti za kimtindo, kimuundo, na kimaudhui katika vipindi tafauti vya kihistoria ambavyo jamii imevipitia.

Hivyo ni wazi kuwa, kila mwaandishi hutafautiana na mwenziwe, na kila kipindi cha kihistoria huwa na fasihi yake. Fasihi ambayo hubeba mtindo wake, huonesha muundo wake na maudhui tafauti kulingana na mahitaji ya jamii kwa wakati huo. Matukio yanayoibuka katika jamii, huisukuma fasihi kufuata mwelekeo huo. Yawezekana kazi ya fasihi ikaandikwa wakati tukio linaendelea kufanyika ama ikaandikwa baada ya tukio kupita. Kwa mfano Giza, Jilala, (2003) na Ushuhuda wa Mifupa, Ngozi, (1992) katika suala la UKIMWI; au baada ya Vita vya Kagera, Zawadi ya Ushindi, Mtobwa, (1992) na Lina Ubani, Mlama (1984).

Muhtasari wa Maonyesho katika Tamthilia ya Amezidi

Katika tamthilia ya Amezidi, mwandishi ameanza kazi yake kwa kuweka nyimbo iliyoandikwa kutoka katika tamthilia ya Kilio cha Haki ya Alamin – Mazrui, yenye maudhui yanayohusu ukombozi wa wanyonge dhidi ya makabaila wachache wenye nguvu za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Jambo hili linawaweka waandishi hawa kuonekana wanaungana kimawazo, mitazamo yao ya kimaisha na kifalsafa kwa ujumla. Katika kianzio mwandishi ameweka “Wimbo wa Mzee” kwa kueleza kwa muhtasari tu hisia zake kuhusu bara la Afrika lilipo sasa na matumaini yake ya siku zijazo kwa kutumia mafumbo. Wimbo huo unaonesha muhtasari wa maudhui makuu ya tamthilia hii ya Amezidi. Mwandishi hakuanza kwa kuonesha majina ya washiriki katika tamthilia.

Onyesho la kwanza mwandishi anaonesha katika akili ya mhusika taswira na hali halisi ya “Pango”, ni sitiari inayobeba picha halisi ya Bara la Afrika. Anaonesha namna Waafrika wanavyoishi katika hali ya ufukara, umasikini na ujinga unaowakatisha tamaa ya maisha. Anamuonesha Ame na Zidi ambapo Ame amelala usingizi mzito. Zidi anaonekana amevaa suruali iliyochanikachanika makalioni. Katika onyesho hilo hilo, mwandishi anaonesha kuwa, tatizo la njaa linachangiwa na uvivu wa jamii zetu za kiafrika. Kama inavyodhihirika (uk 7) Ame anasema, “Na kwa nini mtu apende kazi? Mungu yupo na ardhi ipo ... na ardhi yenyewe bikra ...” Ametumia maneno matatu yenye maana tafauti lakini yenye kukaribiana kimuktadha: ‘kuamka, kutanabahi, kuzinduka’ kuthibitisha kuwa, ipo haja kwa Waafrika kuiona hali inayowakabili na namna ya kuiondosha.

Katika Onyesho la Pili mwandishi anawaonesha wahusika Ame na Zidi wakiwa wamo katika pango ambalo kwao wao ni kasri lililojaa mapambo ya kila aina. Pia, anawaonesha wako ofisini wakiwa Kama boshi na msaidizi wake. Zidi anaonekana anapiga simu kumuulizia boshi wake na kumpa taarifa ya kutokuhudhuria kwake kazini. Wakati huo huo, boshi anayepigiwa simu naye hajafika kazini kwa muda wa wiki mbili.

Onyesho la tatu, mwandishi anaonesha tendo limo mawazoni mwa wahusika. Zidi ameketi juu ya sofa lisiloonekana na Ame amejifanya Mari. Mwandishi anaonesha vijana wa Kiafrika kama Mari na Zidi walivyoathiriwa na utamaduni wa Kimagharibi. Na onyesho la nne, mwandishi anaonesha tendo limo katika fikira za wahusika. Pango limekuwa shule. Zidi ni mwalimu na Ame ni mwanafunzi. Mwandishi anaonesha hali na mfumo duni wa elimu katika nchi zetu za kiafrika.

Onyesho la tano vilievile, tendo linaonekana liko fikirani. Pango linatumika katika muktadha wa ofisini ambapo Ame ni Boshi na Zidi ni msaidizi wake. Mwandishi anaonesha namna wafanyakazi na mabosi wao walivyo wavivu, wazembe na mafisadi; jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya bara la Afrika.

Onyesho la sita, tendo linaonekana pia limo mawazoni. Muktadha unaooneshwa ni wa ofisini lakini ni muktadha tafauti na onyesho lilopita. Mwandishi anaanza kwa kumuonesha Ame akimtaka Zidi watoke pangoni ili wajinusuru na hatari, yaani wadhifa unaotumika vibaya (uk. 51- 52). Pia, anaonesha uovu wa wafanyakazi walioaminiwa na kupewa nafasi za ukaguzi na uofisa, wanavyoshirikiana kufanya ubadhirifu na vitendo vya rushwa.

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

Onyesho la saba, mwandishi anaonesha tendo linafanyika ndotoni mwa wahusika. Ame anakuwa Mari na kuonekana ameathiriwa kwa kiasi kikubwa na uzungu, hadi kujichubua na kujibadilisha nywele. Mwandishi anatumia sitiari “mti msowera ghaibuni” ulioota katika moyo wake na moyo wa Zidi. Mwandishi anaonesha namna jamii zilivyogubikwa na ujinga huo wa kiutamaduni wa kuiga na kuthamini umagharibi, ambao unawameza, kuwaangamiza na kuwafanya wasijue asili zao na mazuri yao ya kiafrika. (uk. 58 - 67).

Onyesho la nane, tendo limo mawazoni. Mwandishi anaona namna waafrika walivyozidi. Sehemu ambayo inaonesha kuzidi kwa uvundo - mambo mabaya, ingawa wengine hawausikii. Uvundo huo ni uvivu, maradhi, utegemezi, n.k, ambao mara nyengine, huchangiwa na waafrika wenyewe. Na onesho la tisa, mwandishi anaonesha tendo linatokea mawazoni. Anaonesha ubadhirifu wa fedha unaofanywa na viongozi kwa kutukuza sherehe sherehe zisizo na msingi na zenye kugharimu pesa nyingi sana. Katika onesho hili kifo cha Zidi kinatokea.

Onyesho la kumi, mwandishi anaonesha tendo linafanyika mawazoni na katika uhalisi- pangoni. Anabainisha kuwa hapa pangoni ni Afrika. Na sauti inasisitiza kuwa ni kuzimu, akiwa na maana mahala palipojaa matatizo ya kila aina: ukosefu wa huduma muhimu za msingi kama maji na chakula kutokana na uvivu na ukoloni mamboleo. Hali hii imewalemaza Waafrika na husubiri misaada yenye masharti magumu kutoka Ulaya. Hatimae ni kifo cha Ame. Na mwisho tamthilia inamalizia kwa nyimbo (Kimalizio).

Muhtasari wa Maonyesho katika Tamthilia ya Mbaya Wetu

Mwandishi wa Mbaya Wetu ameanza kwa kuonesha majina ya wahusika na kuendelea na maonesho moja kwa moja. Katika tamthilia hii mwandishi hakutumia nyimbo mwanzo wala mwisho wa tamthilia kama ilivyo katika Amezidi, isipokuwa mwandishi ameonesha mbinu ya usemi wa pamoja kwa wahusika wote waliopo katika muktadha aliotumia. Mfano (uk. 7, 56, 70), mwandishi ametumia mbinu hii kuonesha unafiki wa baadhi ya raia ambao wote wanakumbwa na matatizo yaliyo sawa lakini badala ya kukaa na kuamua kitu kwa pamoja wengine hugeuka kuwa wanafiki kutokana na kitu kidogo tu wanachodanganyiwa. Nyimbo imetumika (uk 71) na mashairi (uk 55) yanayoimbwa na wahusika.

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

Katika onyesho la kwanza, mwadishi anaonesha nyumbani kwa Fiona, kundi la wanakijiji wanakunywa pombe haramu, buzaa na changaa, huku wakilumbana hadi alipofika Matari na kuanza kufurahia kufika kwake. Ukarimu wa kilevi, wa kuwakirimu kila afikapo sehemu hiyo, ndio sababu ya kusherehekeka kwake. Mwandishi anaonesha namna Matari alivyoiba pesa za dada yake na namna Lila anavyoingia ghafla kwa hasira kumtafuta Matari.

Onyesho la pili, linaonesha ugomvi wa Lila na Matari unaendelea hadi nyumbani kwao huku wakijizuia ili mama yao ambaye ni mgonjwa asisikie. Hata hivyo, mama alisikia na kudakia kwa kuanza kumnasihi mwanawe aache tabia hiyo. Wakati huo pia, Temba anaingia nyumbani kutoka mjini kununua vipuri vilivyoibiwa na Matari na kumaliza mazungumzo kati ya Lila na Temba kuhusu kukusanya kodi ya nyumba zake. Onyesho la tatu mwandishi anaendelea kuonesha mazungumzo kati ya Lila na Temba kuhusu kodi na baadae kuunganisha kuhusu wizi wa Matari, kumuibia kaka yake Tonge.

Katika onyesho la nne mazungumzo kuhusu wizi wa Matari na familia yake yanaendelea kati ya Mtu I na Mtu II. Lila anajibanza chini ya mti kusikiliza kinachoendelea kuzungumzwa. Vero anatokea huku Mtu I na Mtu II wakimpumbaza kwa kumsifu na kujifanya kuwa wanamuona ni mtu mwema ili wapate kugaiwa pesa. Vero anakutana na Lila na kujadili kwa ufupi mazungumzo ya Mtu I na Mtu II, na mwisho wanagombana na kila mmoja kuelekea upande wake.

Onyesho la tano mwandishi anaonesha mvutano uliopo kati ya Tonge na baba yake Temba uliotokana na wizi wa Matari aliyewekwa ndani. Temba anamtaka Tonge amsamehe Matari lakini Tonge anakataa. Pia kupitia tukio hilo Askari I na II wanapata fursa ya kuomba rushwa.

Onyesho la sita, Mama na Lila wako nyumbani kwao. Mama anamtaka Lila asiingie ndani mpaka akamtafute Matari. Temba anaingia na baadae Tonge. Mama anaendelea kumlalamikia Temba na kisha Tonge kwa kumfungisha Matari. Wakati malalamiko yanaendelea yanakatishwa na hodi ya Bi Mkubwa aliyekaribishwa na kuzungumzia kuhusu kulipa fidia ya ng'ombe kutoka kwa watu wa Jefule, muuza nyama aliyenunua nyama ya wizi kutoka kwa Matari.

Onyesho la saba ni mwendelezo wa hadithi. Linaonesha shamrashamra zinazofanyika nyumbani kwa Temba. Mama anaonekana ni mwenye furaha,

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk



anamwagiza Lila kuwaambia wapishi wapike vizuri wali wa dhifa ya kuachiliwa huru kwa mtoto wake Matari. Huku kukiwa na mabishano kati ya Mama na Temba, ambaye hataki kuchinjwe mbuzi kwa sherehe hiyo. Kabla ya sherehe kuanza, Matari anaingia huku amebeba gunia la nguo za wizi.

Onyesho la nane mwandishi anaturejesha nyumbani kwa Fiona, ulevini. Matari anapokewa na walevi wenzake kwa furaha kubwa na kuimbiwa nyimbo ya hongera ikiongozwa na Fiona. Baada ya makaribisho, alionesha ukarimu wake wa kilevi. Alisimulia namna alivyomudu kuiba kwenye nyumba za askari, wakati alipotolewa kutoka jela na kupata pesa za kufanyia takrima hiyo. Baada ya muda, Matari na Fiona wanadaiana pesa na kuingia ndani. Mara, Fiona anapiga kelele anabakwa.

Onyesho la tisa ni la mwisho. Linaanzia nyumbani kwa Temba. Mjakazi anambembeleza Mama kunywa sharubati, kisha Mama na Lila wanajadili kuhusu kukamatwa kwa Matari na kupelekwa mahakamani. Mwisho, tunaoneshwa mahakamani. Hukumu inaendeshwa na Matari anahukumiwa miaka ishirini jela na viboko vinne kwa kosa la kuiba kwa kutumia nguvu na ubakaji.

Ulinganishi wa Vipengele vya Fani

Muundo: Senkoro (2011) anaeleza kuwa, muundo wa kazi ya fasihi ni mpango na mtiririko wa kazi kwa upande wa visa na matukio. Muundo unaweza kuwa ni wa moja kwa moja au wa kiuchangamano. Maelezo yanayoshabihiana na ya Madumulla (2009), anayeeleza kuwa, muundo katika kazi ya fasihi ni mjengo au umbo la kazi inayohusika. Muundo katika tamthilia hizi unatafautina. Sababu kuu ya tafauti hizi ni mikabala iliyotumika katika uandishi wa tamthilia hizi. Mbaya Wetu imetumia muundo wa moja kwa moja, lakini Amezidi imetumia muundo uliochangamana uliokosa muendelezo wa matukio.

Msuko/ ploti: Cuddon (1979) anaeleza kuwa, ploti ni ramani, kielelezo, au sampuli ya matukio ya kazi za fasihi na vilevile ni mpangilio wa kisa na mhusika kwa namna ambayo itachochea udadisi na taharuki kwa hadhira na msomaji. Katika mwendelezo wa nafasi/ wakati katika ploti, kuna swali ambalo hujitokeza katika nafsi (njeo) tatu za wakati. Mawazo ambayo yawiana na ya Foster (1927) anayesema, Ploti ni usimuliaji wa matukio huku mkazo ukiwa kwenye kisababishi. Naye Madumulla (2009), anaonekana kuunga mkono fasili hizo kwa kuelezea msuko kuwa ni mjengeko wa kazi za fasihi ambao unaonesha namna mtiririko wa

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk



mawazo unavyopangwa na mwandishi huku akisisitiza usababishi unaoliwezesha tukio moja kuibua jengine.

Tamthilia ya Amezidi imejengwa kwa maonyesho kumi. Mwandishi wa Amezidi ameibuni kazi yake ikiwa katika vipande vipande ambavyo havina urejelezi, wala si wa moja kwa moja. Matukio katika tamthilia ya Amezidi hayaonekani kuwa na mtiririko. Tunaweza kusema kuwa hayana usababishi. Kila tukio moja linajitegemea. Hakuna muunganiko kati ya tukio moja na jengine. Kila tukio katika onyesho moja haliungani na tukio katika onyesho linalofuata. Pia, mwandishi anaonesha matendo yote yanatokea ndotoni au mawazoni mwa wahusika. Jambo hili halipatikani katika Mbaya Wetu.

Matukio katika Mbaya Wetu yapo katika uhalisi. Tukio tangulizi linaonekana kusababisha kuibuka kwa tukio jengine. Matukio katika maonyesho yote yanategemeana na kukamilishana na kuyafanya yafahamike kwa wepesi na vizuri ukilinganisha na yalivyo katika Amezidi. Hivyo tamthilia hizi zinatafautiana sana katika msuko wake.

Hali hii inatokana na mbinu pamoja na mkabala uliotumika katika uandishi wa tamthilia hizo. Amezidi imetumia mkabala wa kiubwege na Mbaya Wetu mkabala wa uhalisia. Kila Mkabala una misingi inayotafauti na hivyo kumlazimisha mtunzi kutumia misingi maalum ya mikabala husika. Kwa mfano, tamthilia ya Amezidi imetumia mkabala wa kiubwege wenye sifa za udhanaishi. Na ili mbinu ya ubwege ikamilike ni lazima itumike ploti iliyoachana. Ni mazungumzo yanaonekana kutokuwa na mantiki, matumizi ya ndoto, fikra zipitazo akilini mwa wahusika na nyenginezo za kiubwege kwa lengo la kukamilisha ujumbe anaotaka kuutoa na falsafa yake kuhusu maisha.

Vilevile, katika tamthilia ya Amezidi, mwandishi anaonekana kutumia musuko ambao haujaoeleka katika tamthilia za Kiswahili. Ameanza kwa dondoo kutoka katika Kilio cha Haki, ambayo ukiiangalia inakupa taswira nzima ya maudhui ya tamthilia hii. Kisha kufuatiwa na wimbo (Wimbo wa Mzee) uk. 1- 3; na pia ametumia tena wimbo katika uk. 29-30; (Wimbo wa fahari na makuu), uk. 35- 37; (Tajiri Kasimama), uk.72 73; (Usingizi Mtamu) na pia kumaliza na wimbo katika uk.90- 91, (Wimbo wa mtoto asiyezaliwa). Nyimbo hizi zote ni muhimu sana, kwani zimebeba ujumbe maalumu. Kwa mfano, mwandishi anaonesha namna viongozi wazee walivyojishau licha ya kuwa walishuhudia ukoloni na harakati zote za kudai

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

uhuru; namna walivyoshindwa kutimiza ahadi zilizowekwa wakati mkoloni alipotimuliwa. Pia wimbo wa usingizi unaonesha uvivu na ujinga wa viongozi wa Afrika unavyokwamisha maendeleo. Licha ya utajiri mkubwa uliomo katika bara la hili la Afrika, bado waafrika wanategemea misaada kutoka bara la Ulaya na Amerika. Wimbo unaeleza, viongozi wamelala hali ya kuwa wa macho. Utegemezi huo ni usingizi mkubwa.

Katika tamthilia ya Mbaya Wetu kuna maonyesho tisa ambapo matukio yake yanaonekana kushikana. Kila onyesho linaonesha kuwa na mfungamano na onyesho lililotangulia na usababishi wa kuibua tukio jengine; mbinu ambayo haipatikani katika Amezidi. Visa na matukio katika Mbaya Wetu ni yenye kutegemeana. Kuanzia onyesho la kwanza hadi la tisa. Na kunaonekana kuweco kwa muendelezo wa hadithi kiasi ambacho kuondoka kwa onyesho moja kungeathiri sehemu kubwa ya tamthilia hiyo, kuanzia mwanzo hadi mwisho wa tamthilia. Kwa mfano, mlolongo wa visa na matukio ya ulevini vikiambatana na wizi alivyokuwa akivifanya Matari vilimalizia kwa kukamatwa kwake, kupelekwa mahakamani na mwisho kuhukumiwa kufungwa jela. Na kama ingelitokezea kutolewa onyesho na. 5 ama na. 8, tamthilia hiyo ingelikosa mtiririko mzuri wa visa na matukio unaoiendeleza hadithi katika tamthilia hiyo.

Wahusika: Wahusika ni watu ama viumbe waliochorwa katika kazi ya fasihi waliokusudiwa wawakilishe dhana, wazo au tabia za watu katika kazi ya fasihi. Huchorwa kwa fikra (maneno) kwa msingi wa kitamaduni na hivyo huweza kufahamika zaidi kwa wepesi kwa jamii husika.

Katika kipengele hiki tunapata mfanano na tafauti. Tukianza na tafauti tunaona kuwa, katika Amezidi, mwandishi ametumia wahusika wawili; Ame na Zidi tu ambao amewabebesha nafasi tafauti. Kwa mfano, katika Onesho la tatu (uk 20- 25) mwandishi ametumia wahusika Zidi na Mari. Ame anachukua nafasi ya mwanamke yaani mpenzi wa Zidi anaaitwa Mari. Pia katika Onesho la Tano (uk 43-50) mwandishi anamuonesha Zidi na Ame katika nafasi nyengine kama, mfanyakazi na bosu wake (Bosu na Msaidizi). Katika Onesho la saba wahusika Ame na Zidi, kwa mara nyengine wanaoneshwa katika nafasi ya mtu na mpenzi wake. Ame anakuwa Mari na Zidi ni mpenzi wake. Mwandishi anazitumia nafasi hizo kusimamia dhamira tafauti.

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk



Mohamed amewasawiri wahusika wake vizuri sana, kwani amewatambulisha na kuwachora kimajazi. Unapoyaunganisha majina haya ya wahusika, Ame na Zidi, tunapata msamiati“amezidi” neno linalosimamia anuani ya kitabu na kuakisi tabia ya wahusika hawa vizuri ambao wanaowakilisha wananchi na viongozi wao ndani ya bara la Afrika. Neno hili limetumika kiistiara, linalandana na kuwiana na hali ya kuzidi kwa tabia mbalimbali zinazorudisha nyuma maendeleo ya nchi tafauti barani Afrika. Tabia kama vile uvivu, rushwa na ubadhirifu wa mali ya uma kwa visingizio vya semina na makongamano yasiyo na tija. Mipango mibovu ya kimaendeleo isiyo na utekelezaji, utegemezi na kadhalika.Vyote hivyo vinaonekana na mwandishi kuwa vimezidi mno katika nchi zetu.

Kwa upande wa Mbaya Wetu, mwandishi ametumia wahusika wengi ukilinganisha na wahusika wa Amezidi. Katika tamthilia hii kuna wahusika kama vile, Mtu I, Mtu II, Mtu III, Matari, MzeeTemba, Mama, Lila, Tonge, Vero, Fiona, Jefule, Mjakazi, Bi Mkubwa, Askari I, Askari II na Wanakijiji. Wahusika hawa wamebebehsa dhima maalum zinazosimamia dhamira mbalimbali kama, madhara ya ulevi, wizi, malezi mabaya, utabaka na nyenginezo.

Tafauti nyengine iliyojitokeza ni kuwa, mwandishi wa Amezidi ametumia wahusika wakuu wawili Ame na Zidi tu. Yaelekea kuwa, lengo lake ni kuonesha na kusisitiza mtazamo wake juu ya kukithiri kwa hizo tabia alizotaka kuzionesha. Katika Mbaya Wetu mwandishi metumia mhusika mkuu mmoja tu, Matari ingawa wote lengo lao ni sawa ambalo ni kuonesha uoza uliokithiri katika jamii za Kiafrika. Hali hii ni kutokana na kuathiriana kwa jamii kutokana na matendo mabaya ya wanaadamu ndani ya jamii zao, hivyo waandishi wote wameandika kwa lengo la kuzikosoa jamii zao.

Tukurudi upande wa mfanano, wahusika waliotumika katika tamthilia ya Mbaya Wetu ni wahusika halisi kama ilivyo katika tamthilia ya Amezidi. Katika onyesho la tisa, baadhi ya wahusika wamekamata nafasi nyengine, kama vile, Mama ameshika nafasi ya hakimu, Tonge ameshika nafasi ya wakili wa Matari na Temba ni askari. Mbinu hii ni kama ile inayopatikana katika Amezidi katika onyesho la tatu, nne, tano na saba. Hivyo, katika kipengele hiki waandishi hawa wawili wanafanana kwa kutumia wahusika halisi na pia wahusika kubeba nafasi zaidi ya moja.

Pia tamthilia zote zimetumia wahusika wa kimajazi. Katika tamthilia ya Amezidi, mwandishi ametumia mchanganyiko wa majina ya Ame na Zidi yaliyojenga

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

neni 'amezidi', linalorejelea kuzidi kwa matendo yanayorudisha nyuma maendeleo ya jamii. Kwa mfano, mwandishi anaonesha hali ya kuzidi kwa uvivu, uzembe na utegemezi na mambo mengine yanayorudisha nyuma maendeleo ya nchi zetu za kiafrika.

Katika Mbaya Wetu mwandishi ametumia Matari, kwa maana ya mburumatari, mwenye akili mbovu, mtu hohehahe, mtu wa hali ya chini kimaadili, aliyekosa heshima, ukilinganisha na familia yake ilivyo. Familia yake ni ya watu wastahiki walio katika tabaka la juu. Lakini yeye alikuwa ni mtu ovyo na mwenye tabia mbaya, kama, wizi na ulevi.

Vilevile, katika kazi zote mbili waaandishi wametumia wahusika wakuu bapa. Wahusika wasio badilika kitabia. Katika Tamthilia ya Amezidi, wahusika wanaonekana kuanzia mwanzo hadi mwisho ni watu walio na tabia za kinjozi, wenye mawazo finyu yasiyo na mtazamo angavu unaomulika mbele kimaendeleo. Mazungumzo yao yote yamejaa vipengele vya uvivu, ubadhirifu, ombaomba, ubwege na udumavu. Kwa mfano, Ame anasema, "Na kwa nini mtu apende kazi? Mungu yupo na ardhi ipo. . . na ardhi yenyewe ni bikra . . ." (uk. 7). Dondoo nyengine inayothibitsha hali hiyo inapatikana katika mazungumzo ya Ame anaposema " Umeshapeleka maombi ya msaada huko umoja wa mataifa? Au kuomba ruzuku nchi za magharibi yaani EC?" (uk. 9)

Katika (uk. 9) pia tunapata dondoo inayoonesha ufinyu wa mawazo ya kimaendeleo ya wahusika hawa, pamoja na utegemezi.

Ame: Aaaa, shida yote ya nini bwana. Kabla kibiriti hakijavumbuliwa wazee wetu walikuwa wakifanya nini?

Zidi: Wakipekecha moto

Ame: Ha, ha, ha...(Anacheka kwa nguvu) Karne ya ishirini hii; leo tupekeche moto na vibiriti kutoka uchina vipo vimejaa..." (uk 9).

Dondoo nyengine inayothibitsha mawazo yasiyo na mwamko wa kimaendeleo inaonekana katika (uk. 35) ambapo mwanafuzi anasema:

Mwanafunzi: Tatizo... Hapana... ngoja kwanza . . .(Anacheka). Si tatizo uzuri ni

kwamba . . . ni kwamba tu matajiri, na tajiri hana haja ya kufikiri, anaweza kuwalipa watu, wengine wamfikirie, wamfanyie utafiti, wamvumbulie. . ." (uk. 35). Tabia kama hizi za wahusika pia zinajitokeza katika uk. 45, 56, 64, 70, 77, 87, ambapo mawazo ya wahusika na matendo yao huoneshwa katika miktadha tafauti. Na kila muktadha unaonesha wazi tabia hizohizo zisizobadilika za kutokuwa na fikra za kimaendeleo ya kiuchumi wala kisiasa.

Mandhari: Katika kipengele hiki, waandishi wote wawili wametumia mazingira yanayoakisi uhalisi na hali halisi ya nchi za kiafrika ingawa kuna tafauti ya ujengaji wa mandhari hizo kwa baadhi ya matukio. Katika tamthilia ya Amezidi mwandishi anatumia mandhari za kufikirika kwa wahusika wake. Mandhari zimechorwa katika miktadha tafauti inayooneshwa inapita mawazoni mwa wahusika. Hata hivyo, hujenga taswira za uhalisi kwa msomaji wa kazi hii. Kwa mfano, wahusika wanahisi kuwa wamo katika kasri ilihali wamo katika pango. Wakati huohuo, msomaji anapata picha ya mandhari halisi ya kasri anaposoma. Mwandishi ametumia mandhari za aina hiyo ili kuyasawiri vyema matendo ya wahusika aliowachora. Amechagua aina hiyo ya mandhari kusimamia dhamira alizotaka kuzionesha katika tamthilia hiyo kama inavyooneshwa katika uk. 13.

Ame: Kama umepata kuikagua kwa macho nyumba yetu...

Zidi: Humu pangoni

Ame: Pangoni, au kasrini mwetu?

Zidi: Ah, Kasri ndiyo, kwani lina nini? (uk 13)

Mwandishi wa Amezidi ameonesha mandhari kama hiyo tena katika uk 82 ambapo Ame anaona mafunza yasiyokuwepo.

Zidi: Aaaaaa. (Anapiga usiyahi mkubwa) naona mafunza . . . hayo.

Ame: yako wapi? Mbona mimi siyaoni?

Zidi: Wewe si mfu eti, utayaonaje?

Ame: Mengi mangapi?

Zidi: Bilioni kwa bilioni... yako ukutani, yako masofani, yako zuliani,

yako vitini yanafunika kila kitu . . . ishara gani? ...

Vilevile, mwandishi ameonesha muktadha wa shuleni kwa lengo la kuonesha mfumo wa elimu unaoendeshwa na mataifa mengi ya kiasia ikiwemo Tanzania.

Mwalimu: Na . . . na . . . atataja Archimide's Principle . . . enhe (Kwa mwanafunzi Ame) wewe Ame! (Sasa mwalimu bakora ndefu) . . .

Mwanafunzi: Hivi . . . hivi kukariri mawazo ya Archimide's kuna faida gani? . . .

Mwanafunzi: Hivi . . . hivi baada ya kukariri mawazo ya Archimide's kwa miaka mingi kwa nini hatujaweza kuunda nyambizi?... (uk 32)

Muktadha mwengine ni wa ofisini. Mwandishi ametumia muktadha huo ili kuakisi utendaji mbaya kama kutokuwajibika kwa wafanyakazi na mazingira yanayochochea rushwa. Katika muktadha hiyo ya ofisini, kwanza anaonekana Mchunguzi wa mahesabu – Zidi anaandaa vinywaji ili kumlainisha mkaguzi. Mwandishi amejenga mandhari hiyo kuonesha uoza unaoanywa katika jamii. Ofisi hiyo inawakilisha muktadha wa wizi na ubadhirifu katika ofisi za umma. Kama inavyothibitishwa katika onyesho la sita, uk 56.

Ame: Ngoja nikuburudishe kidogo . . . hutaki burudani wewe?

Zidi: Burudani!

Ame: Ngoja!

Zidi: Vizuri (Anaonekana kufungua friji lisiloonekana na kutoa chupa... na glasi mbili zisizoonekana. Anarudi) Zidi: Ice cubes? (uk 56)

Mazingira kama hayo ya rushwa na ubadhirifu katika maofisi ya umma huonekana tena katika muktadha wa ofisi hiyo hiyo. Mwandishi analidhihirisha jambo hilo katika dondoo hapo chini.

Ame: Kwa nini nisiingiwe na hofu na wewe ni mkaguzi wa mahesabu ya serikali?

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

Zidi: Lakini ndugu yako.

Ame: Aaa kweli. . . (Anakumbuka) hata nilisahau kwamba wewe ndugu yangu. . . Na ndugu?

Zidi: Hawalani wala hawaumani. . .

Ame: Badala yake?

Zidi: Huhifadhiana . . . hupendana . . . husaidiana ukila wewe na ndugu yako mpe, ndio uhuru, kujitawala huko, kujitawala ndugu kwa ndugu, watoto wa shangazi na mjomba . . . Alipokuwepo mkoloni tuliweza kufanya haya?. . (uk 56)

Pia uzembe unaofanyika katika ofisi za umma unathibitishwa katika uk 16. Matendo kama haya anayoyaeleza mwandishi wamekuwa yakitendeka kila siku katika jamii. Kama dondoo hapo chini inavyoonesha.

“ . . . Ah sekretari . . . Joyce? Bosi hayupo?

Ee . . . hajaja wiki ya pili sasa? Anaumwa . . .

Hapana sicheki kitu . . . ndiyo mambo yanavyokuwa kazi na dawa . . . tumejitawalaati siyo kujituma tu . . .

Ah, O/D? cheti cha daktari Enn, kuthibitisha ndiyo, sawa nitaleta kama kawaida .

. . haya ahsante (uk 16)

Mandhari zote hizo katika miktadha tafauti zimejengwa katika fikra za wahusika lakini inaakisi uhalisi wa jamii zetu; jambo ambalo husababisha kuongezeka kwa utegemezi na kutokuwa na umakini katika upokeaji wa misaada.

Kwa upande wa tamthilia ya Mbaya Wetu, mwandishi ametumia mazingira halisi ya Afrika hususan katika nchi ya Kenya. Mwandishi ameonesha mandhari ya kijijini katika miktadha tafauti. Kwa mfano, mandhari ya nyumbani, muktadha unaojitokeza ni wa malezi. Katika muktadha huo, mama anaonekana kumdekeza

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

mwanawe kupita kiasi; jambo ambalo linampotosha na kumuingiza katika vitendo vya wizi na ulevi. Mwandishi anauonesha kutokana na dhamira aliyotaka kuionyesha katika kazi yake. Muktdha huo unadhihirishwa katika dondoo ifuatayo.

MAMA: . . . Mwanangu kindakindaki karibu. Inakuwaje watu asioweza kukuumba wanakuumbua?... Lo!... Mungu ni mkubwa umerudi salama mwanangu kindakindaki, mwanangu mziwanda...

TEMBA: Basi endelea kumdekeza adekezwe. Yatakuja kukutokea puani. Wacha nende zangu [Kwa Matari] We' umesikia?[Kimya] nimesema usifanye nini tena? . . . Hata ukunyamaza najua umesikia. Nenda ukachume msiba tena uone kama utaula na watu wa kwenu. . .

MAMA: Matari mwanangu. Hapa ni kwenu. Kula ushibe, ulale usone bila ati ati. Nami leo nitakula chakula kinitue tumboni ati. Njoo. Njoo mwanangu nikupige pambaja kitoto changu. Njoo. (uk 65-66).

Mandhari nyengine ni ya nyumbani kwa Temba ambaye ni tajiri katika kijiji hicho. Mandhari hiyo inabainisha wazi hali inayoonyesha utabaka ulioko katika jamii iliyoandikiwa. Kwa mfano, mwandishi anaonesha utajiri wa Temba kupitia mhusika MTU 1 NA MTU 11. Katika mazungumzo hayo inaonekana kuwa ni mtu asiye na mlahaka mzuri kwa wenziwe.

MTU 1: Wala mimi sioni ajabu, Hiyo aila ya Temba wanapenda kujinaki kuwa wao ndio watu bora.

MTU 11: Acha wafedheheke, labda wataanza kuwathamini watu. Matari amefanya vizuri Kuwakomoa.

Pia nyumbani kwa Fiona, ni mandhari aliyoitumia mwandishi kuonesha nyumba iliyogubikwa na mazingira ya ulevi. Mwandishi ameweka mandhari hii kudhihirisha ubaya wa tendo hilo la ulevi. Muktdha huu wa ulevi unaonekana umejaa fujo za kila aina. Kama invyoelezwakatika dondoo lifuatalo:

MATARI: Hizo pesa zimekwishaje?

FIONA: Zimekwisha.

MATARI: Zimekwishaje?

FIONA: Tuelewane Matari. Hebu twende ndani tuzungumze chemba, tuelewane. . . .

FIONA: (Anasikika kutoka nje ya jukwaa akipiga usiahi mkubwa) Uwiiiiiii! Uwiii! Wacha kunibaka. Wacha kunibaka. Wacha kuniibia. Nduli wewe. . . Kama wataka kuniua niue.

MATARI: (Kwa sauti kubwa) Toa fedha zangu. Toa huwezi kuzibania hela zangu nilizopata kwa jasho langu mwenyewe. Toa fedha zangu... (uk 73-74).

Mandhari nyengie inayojitokeza katika tamthilia hii ni kituo cha Polisi. Katika mandhari hiyo, miktadha mbalimbali inathibitisha kuweco kwa tatizo kubwa la rushwa, uvunjwaji wa haki za binadamu, ukiukwaji wa sheria na kutokuwajibika. Hali hizo zinathibitishwa na mwandishi kupitia dondoo zifuatazo.

“[Ni eneo la Polisi Jefule na Matari wamo kwenye korokoro ya Polisi.

Askari anaokana ana bunduki na ufunguo. Tonge na babake Temba

wamesimama karibu na Poilisi. Karibu na Askari kuna kibao

kilichoandikwa ilani“HAPA SI PAHALA PA KITU KIDOGO”]. (uk. 46)

Hali hii pia inaoneshwa kupitia mhusika ASKARI 1, anaeleza kama ifuatavyo:

“ASKARI 1: Nilikwambia karandinga halina hata tone la mafuta.....

. . . wataka nikuambie mara ngapi wewe? Labda nyie mtumie

gari lenu “ (uk. 46.)

Katika maelezo haya mwandishi anamuonesha mhusika Askari namna anavyotengeneza mazingira ya kuchukuwa rushwa. Anashurutisha kuwa gari haina mafuta, na yaliyopo yametengwa kwa aina maalumu ya washtakiwa jambo

amabalo halina mantiki. Pia katika suala hili mwandishi anamuonesha askari huyo huyo anaomba rushwa kwa mtindo mwengine kama anavyothibitisha katika sehemu ifuatayo:

ASKARI 1: Kama ni ombi kumbuka mti hawendi bila ya nyenzo. Kama Kiswahili hicho ni kigumu kwa mtu aliyesoma kama wewe basi wacha nikupe kauli rahisi; mkono mtupu haurambwi. . .”

ASKARI 1: Hata kidogo. Kumbe elimu mnayosoma haiwasaidii kitu. Ila ni kidogo tu, inakushinda kuelewa. Maanake hasa ni kwamba hatukubali sisi kitu kidogo; twakubali kitu kikubwa tu. [Anaonesha pesa alizopewa mwanzoni] Hizi hazitoshi. [Tonge anatikisa kichwa kwa hasira] Umesikia? Ongeza. Fanya haraka bwana. Na ukicheza nitakufungulia mashtaka ya kutaka kunipa hongo. [Tonge anatia mkono mfukoni tena na kumwongezea ASKARI 1 pesa zaidi. Kisha anaondoka jukwaani]” (uk 49)

Vilevile, mwandishi ametumia muktadha wa mahakamani ambako kwa kiasi kikubwa kunaonekana kuna mabadiliko. Mahakama inaonekana kujiepusha na upokeaji wa rushwa. Na kusimamia sheria ipasavyo. Ingawa kumejitokeza tatizo la kutokuangaliwa kwa umakini kwa malalamiko ya washtakiwa. Kama inavyodhihirika katika dondoo hapo chini ambapo hakimumu (MAMA) anasema,.

MAMA: . . . Uchunguzi umebaini kwamba mshukiwa ana mazoea ya kuvunja sheria kutokana na kuendelezwa na kutendekezwa na wazee wake. Asiyefunzwa namamaye hufunzwa na ulimwengu. Mahakama hii ni sehemu ya ulimwengu unaojua kufunza. Mahakama hii imekataa hata juhudi za nasaba ya mshukiwa kuihonga ili kubadili mkondo wa haki usiozulika.

Katika kipengele hiki, tunaona kuna tafauti kati ya waandishi hawa. Ingawa wote wameonesha mazingira halisi yanayowakilisha nchi zilizo katika bara la Afrika, katika tamthilia ya Mbaya Wetu mwandishi ametumia mandhari halisi inayoonesha utamaduni ya nchi husika. Kwa upande wa Amezidi mandhari yake ni ya kufikirika

tu mawazoni mwa wahusika. Uhalisi hujengwa na msomaji mwenyewe kupitia taswira anayojenga kutokana na tajiriba ya mazingira halisi aliyonayo. Mandhari na miktadha yote iliyotumika imeakisi mazingira halisi ya nchi za Afrika.

Mtindo: Hiki ni kipengele muhimu katika fani kinachoonesha namna kazi ya sanaa ilivyosimuliwa. Kifaa chake muhimu kinachotumika kujadili mtindo ni lugha. Ni kipengele kinachoifanya kazi ya fasihi kuwa na ufasihi. Senkoro (2011) anaeleza, mtindo ni ile namna ambayo mwanasanaa huipa kazi yake ya fasihi sura ya kifani na kimaudhui ambapo msanii mwengine asingeweza hata kama wanazungumzia kitu kilicho sawa. Mtindo hujumuisha lugha za aina kwa aina, kama tamathali za semi, misemo, nahau, methali, uchunguzi wa misamiati, miundo ya sentensi, ufundi wa kuwachora wahusika au kuwaeleza, mandhari na matukio na hata utamu wenyewe wa lugha itumiwayo. Baadhi ya matumizi hayo ndiyo yatayolinganishwa katika sehemu hii.

Matumizi ya Lugha na Mbinu Nyengine za Kisanaa

Lugha ni kipengele muhimu katika kazi yoyote ya fasihi. Lugha ni daraja inayomuunganisha msanii na hadhira na huifanya hadhira kupokea ujumbe, kuelewa dhamira na kubaini migogoro mbalimbali aliyoikusudia msanii iwafikie wasomaji wa kazi hiyo. Lugha ndio nyenzo kuu inayotafautisha kazi ya fasihi na Sanaa nyengine na ndicho kipimo thabiti kinachomtafautisha mwandishi mmoja na mwengine. Katika Makala hii tutaangalia kwa namna gani waandishi hawa wawili wamefanana na kutafautiana katika matumizi ya tamathali za semi kama tash-biha, tashihisi, taashira, ishara, sitiari pamoja na mbinu nyengine za kisanaa.

Matumizi ya Taswira na Ishara

Senkoro (2010) anaeleza taswira kuwa ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa kutumia ishara. Mkusanyiko huo wa picha ya kimawazo hujengeka kutokana na masimulizi ya kisanaa yaliyo dhahiri na yenye kuvutia fikra. Mara nyingi taswira huambatana na matumizi ya tamathali za semi hasa sitiari na tashbiha. Katika taswira msanii hupanga maelezo yake kiasi cha kuifanya hadhira yake ipate aina mbalimbali za hisia za kunusa, kusikia, kuona, kuonja na kugusa. Waandishi hutumia taswira ili kuzifanya kazi zao ziwe hai zaidi; hutumia kunasa hisia za hadhira kwa kupanga maneno yanayoweza kujenga picha kamili katika hisia zao. Mara nyingi taswira hizi huongeza uzito wa maudhui ya kazi za fasihi kuhusu maisha.

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk



Matumizi ya taswira mara nyingi huambatana na ishara. Ishara hizo huwa ni dhana au mawazo yanayotumiwa na waandishi kuwakilisha, vitu , dhana au mawazo mengine. Ishara ni dhana muhimu sana katika kubuni kazi ya fasihi. Nauta (1972) ana maoni kwamba ishara huwakilisha kifikira hali ya kitu kinachoashiriwa na kwamba uhusiano wa ishara na kiwakilishwa ni wa kidhahania.

Madumula (2009) anasema, “neni ishara kama istilahi ya kifasihi, ni lile lililo sawa na neno la Kiingereza la ‘symbol’. Anaongeza kuwa neno ‘symbol’ linatokana na neno la Kiyunani ‘symbolon’ ambalo ni kitenzi chenye maana ya ‘tupia pamoja’ na nomino yake ni ‘symbolon’ kwa maana ya ‘alama’, ‘nembo’ au ‘dalili’ au ‘ishara’. . . Ishara huwakilisha kitu au hali halisi pasipo na ulazima wa kufanana. Huwa na asili katika tamaduni mbalimbali.”

Anatahadharisha kuwa katika fasihi, msanii anaweza kutumia vitu fulani kusimamia ishara zake mwenyewe na kwa makusudi yake binafsi na kwa kufanya hivyo, akawa amekiuka maana zilizozoeleweka au za kiutamaduni.

Wamitila (2003) anpozunguzia ishara na uashiriaji, anaeleza kuwa, ishara hutumiwa kuelezea kitu fulani ambacho huwakilisha kingine katika uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au uwezo wake wa kuibua fikira fulani katika akili ya msomaji. Hivyo ishara huchukua muundo wa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, vitendo au vitu halisi. Kitu chochote hakiwezi kuwa ishara kama hakitafasiriwa kama ishara. Ishara kama kitu tunachokumbana nacho moja kwa moja huweza kuashiria kitu chengine tafauti. Maneno huchukuliwa kuwa ishara kwa sababu hupewa maana na watu wenyewe.

Waandishi wote wa tamthilia hizi, wametumia taswira na ishara isipokuwa katika Amezidi taswira na ishara zimetumika kwa wingi zaidi kuliko katika Mbaya Wetu. Taswira na ishara zilizotumika katika Amezidi ni kama, muhogo uliovunda, mafunza yaliyotapakaa, pango, mti msowera, kasri, ugaga, kiza, nyama iliyooza. Misamiati hiyo yote imetumika kiishara. Tafauti hizo zimetokana na dhamira walizokusudia kuzieleza katika tamthilia zao. Kwa mfano, mwandishi anasema katika Wimbo (uk 72):

Kiza tunakisherehekea

Kiza kitamu kiza

Kitamu kiza kitamu

kitamu kwa sababu

tumelala usingizi Mnono. (uk 72)

Katika dondoo hii mwandishi ametumia neno kiza kuwa ni ishara inayoashiria ujinga walionao Waafrika. Pia ametumia neno ugaga kama inavyoonekana katika (uk 22).

Mari: Unajicheka kwa uzembe wako enh!

Zidi: mbona sihisi?

Mari: Una ugaga wa hisia eti?

Ugaga unaashiria mtu asiye na mawazo mapya ya kimaendeleo. Nyama iliyooza huashiria misaada mibovu inayosababisha maafa katika nchi, Mafunza yametumika kuashiria madhara yanayotokana na misaada ambayo huathiri nchi nzima. Mwandishi ametumia ishara hizi kwa lengo la kusimamia dhamira alizokusudia kuzionesha. Taswira nyengine anayoieleza mwandishi ni mafunza yaliyotapakaa. Kwa mfano,(uk 80- 84).

Kwa upande wa Mbaya Wetu, mwandishi ametumia taswira tafauti. Kwa mfano, ametumia taswira ya kimaelezo kuonesha namna mhusika Vero alivyojibanza huku akisikiliza mazungumzo kati ya MTU 1 na MTU 11, katika uk 35, 36.

“...hawajamwona Lila akijitokeza. Lila anasita mwendo kidogo. Anawaza na kuwazua kama aendelee na safari au asiendelee. Hatimaye anajibanza nyuma ya mti na kujikunyata anawaona ilhali wao hawamuoni. Anawasikia ilhali wao hawamsikii” (uk 35).

Kupitia dondoo hii msomaji hupata picha namna mhusika Vero alivyokuwa amejificha chini ya mti bila kuonekana. Taswira kama hii hujenga picha na haina maana nyengine ya ziada.

Pia mwandishi ametumia taswira ya kiishara, wakati wa mazungumzo ya mhusika Fiona na Mtu 11 waliokuwa wanazungumza kuhusu kuachiliwa kwa Matari na Jefule. Fiona anamwambia Mtu 11.

Fiona: Wewe waishi sayari gani?

Mtu 11: Kwa nini?

Fiona: hujasikia ukoo wa Jefule umetoa fidia Matari na Jefule wakaachiwa huru?

Mtu 11: Lo! Simba wameachiwa tena kuingia kwenye msitu wa kondoo. (uk 70).

Katika mazungumzo hayo tunapata picha nzima ya simba na kondoo katika akili na mamna wanavyokuwa katika msitu. Simba ametumika kuashiria mtu hatari anayedhuru watu wengine. Na kondoo wanaashiria watu wengine wanaofanyiwa vitendo vya kikatili ama kudhuriwa.

Katika tamthilia hiyo pia tunapata taswira ya kiishara inayoeleza juu ya ubaya wa Matari wa kumuibia kaka yake mali pamoja na mkewe.

MTU 1: Wa wanasemahiyo mimba ya mkewe Tonge ni ya Matari.

Ati Matari husubiri nduguye akienda mjini kufanya kazi, basi naye akenda kurusha ndege kwenye anga za wenyewe.

MTU 11: (Anapigwa na butwaa) Uongo!

MTU 1: Ni kweli yakhe. Wewe unafikiri Tonge anaweza kumtungisha mwanamke mimba?(uk 36)

Katika mfano huo, kishazi kurusha ndege ni tasahira, na kwenye anga za watu ni taashira iayoashiria kuzini na wake za watu.

Methali

Katika tamthilia ya Amezidi mwandishi ametumia methali kama vile, 1. Nyani haoni ghubaye (uk 5) 2. Aliyemo hatoki na asiyekuwemo haingii, (uk 49). Mwandishi hakutumia methali nyingi kama zilivyotumika katika Mbaya Wetu; hivyo kuna tafauti inayojitokeza.

Katika Mbaya Wetu mwandishi ametumia methali nyingi zaidi kama vile:

1. Ndugu wakigombana chukua jembe ukalime wakipatana chukua kapu ukavune, (uk 16).
2. Maji yakimwagika hayazoleki,(uk 46).
3. Meno ya mbwa hayaumani, (uk 46).
4. Mti hawendi bila ya nyenzo, (uk49).
5. Mkono mtupu haurambwi. (uk. 49).
6. Maji nimeyavalia nguo sharti niyakoge, (uk 48).
7. Mwenda tenzi na omo marejeo ni ngamani, (uk 67).
8. Usimuamshe aliyelele ukimuamsha utalala wewe, (uk 69).
9. Nenda ukachume msiba uone kama utaula na wa kwenu, (uk 66).
10. Mgema akisifiwa tembo hulitia maji, (uk 69).

Mwandishi ametumia methali hizi kwa lengo la kuonesha maadili ya jamii pamoja na matuko yanayodhihirisha mfumo wa amali za kijamii. Pia mwandishi ametumia methali hizi kujenga mandhari ya kitamaduni inayoaminika katika jamii iliyohusika kama vile kutumika kutoa maonyo ama tahadhari anayopewa mtu ndani ya jamii hiyo. Hivyo, kila methali inasimamia dhamira maalum. Kwa mfano, katika methali Na. 3 hapo juu, mwandishi amemtumia mhusika Temba akiwa katika mjadala mzito kati yake na Tonge ambapo Temba anataka Tonge amsamehe Matari kutokana na kosa la wizi alilotenda. Hali hii inasaidia kujenga maelewano na mapenzi ndani ya jamii kama anavyoonesha mwandishi katika (uk 46).

” TEMBA: Kama kuibwa ng’ombe kaibwa. Kama kuchinjwa ng’ombe kachinjwa. Ungeyaachia tu hapa mwanangu. Maji yakimwagika hayazoleki. Tena meno ya mbwa hayaumani.”

Maneno ya Temba hapo juu yanaonesha kuwa, anakiri kuwepo kwa kosa lakini hapana budi aliyekoswa asamehe. Anaona kwamba, hata kama kosa limefanyika

ni vyema pia kusameheana kwani hao ni ndugu na daima ndugu hawapaswi kugombana.

Na katika methali Na. 6, mhusika Tonge anaonesha msisitizo juu ya msimamo wake. Kwa kusema:

TONGE: Maji nimeshayavulia nguo sharti niyakoge.”

Kauli hii inaonesha kuwa Tonge ameshaamua katu hatomsamehe ndugu yake. Ni lazima amshitaki kutokana na kosa alilomtenda. Mwandishi ametumia methali hizi kuonesha maadili na mazingira ya jamii yanayojenga uhalisi wa jamii kwa kuiaminisha hadhira yake kwamba matukio kama hayo hujitokeza katika jamii.

Tafauti inayojitokeza katika matumizi haya ya methali kati ya tamthilia hizi inatokana na aina ya tamthilia zenyewe. Amezidi ni tamthilia iliyoegemea zaidi katika thieta ya ubwege, haikujikita kuonesha maadili ya jamii hasa malezi. Imezingatia zaidi mifumo ya kiuchumi na dhamira nyeti za kisiasa. Hivyo ni tamthilia iliyozungumzia maudhui nzito zaidi na kwamba methali zilizotumika ni chache na zimejengwa zaidi kikejeli.

Kwa upande wa Mbaya Wetu ni tamthilia iliyoegemea zaidi kwenye mtazamo wa jamii hususan malezi pamoja na mfumo wa kiuchumi katika historia ya nchi ya Kenya. Tamthilia za aina hii hulazimika kutumia methali nyingi zaidi kwa lengo la kuonya na kuadibu dhidi ya malezi katika jamii, pamoja na mgawanyiko uliopo ndani ya jamii. Hivyo tafauti hizi zimejitokeza zaidi kutokakana na maudhui ya kazi hizi- dhamira pamoja na ujumbe aliokusudia mwandishi kuufikisha katika jamii yake.

Matumizi ya Nahau

Senkoro (2011) anafafanua kuwa, nahau ni msemu unaojengwa kwa maneno ya kawaida lakini huwa umesitiri maana tofauti na ile inayobebwa na maneno hayo katika matumizi ya kawaida. Nahau tafauti zimetumika katika Mbaya Wetu: kwa mfano (uk.4) Mkono wa korosho; (uk. 29) Mja mzito; (uk. 69) na Kula kalenda; (uk 69); kukatika waya (uk 12). Mbinu hii haikutumika katika Amezidi.

Tafauti hii zaidi inatokana na uteuzi wa maneno alionao mwandishi mwenyewe kwa kutumia ubunifu wake kuipamba kazi yake. Pia, kusudio la kuonesha dhamira

maalumu zinazosimamiwa na nahau hizo pamoja na kuzisisitiza kwa kukijengea picha halisi kile anachokizungumza.

Tamathali za Semi

Tamthali za semi ni kipengele chengine kinachotumika katika kuonesha namna waandishi hawa walivyotafautiana au walivyofanana katika kazi zao. Tamathali zitakazoelezwa ni tashbiha, na tash-hisi.

Tashbiha: Tashbiha ni usemi wa mlinganisho unaotumia vilinganishi. Katika Mbaya Wetu mwandishi ametumia tashbiha zifuatazo:

1. Anaanguka kama gunia la viazi. (uk 69)
2. Wape wote hawa wanywe buza ifurike matumboni mwao kuliko gharika ya Nuhu.(uk 72)

Tash-biha hizi zote zinaibua dhamira za athari hasi za ulevi, ambazo huambatana na matatizo. Tamathali na. 1 inaonesha namna mlevi anavyokosa heshima hata kama amevalia vizuri na alionekana mtu wa heshima kabla ya kulewa. Anapolewa anaweza kuanguka ovyo na hata kuvunjiwa heshima.

Tashbiha na. 2 inaonesha athari za ulevi na ulevini. Hali hii hatimae humweka mlevi pahala pabaya kama vile, kupigwa na mara nyengine kufungwa; jambo ambalo linazorotesha maendeleo ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa jumla. Kipengele hiki hakikujitokeza katika Amezidi kwa sababu ya mkabala aliotumia mwandishi. Mkabala wa kiubwege uliofungamana na udhanaishi, umemfanya atumie zaidi sitiari na mafumbo kutokana na uzito wa dhamira alizozionesha.

Tash-hisi: Hii ni aina ya tamathali inayofananisha kitu kwa kukipa kitu kisicho na uhai uwezo wa kibinadamu wa kufanya tendo fulani. Katika Amezidi tash-hisi inaonekana katika, uk. 1 ambapo, mwandishi amelihuisha bara la Afrika kwa kusema, kama kwamba ni kitu chenye uhai kinachoweza kujisimamia na kujifanyia mambo yake kama mwanadamu kama inavyoonyeshwa katika dondoo hapo chini.

“Kwa nini ewe bara la Afrika

Ewe nchi uliyejipamba kwa weusi

Ewe roho ya kizazi chetu

Tukutiliaye mbolea siku baada ya siku

Kwa kutaraji utatuzalia matunda . . .” (uk. 1)

Tash-hisi nyengine ni kama, kicheko kinatucheka nafsi zetu (uk. 86). Kicheko kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Fasaha (2010) ni utoaji wa sauti ya furaha. Hivyo kiumbe chenye uhai ndicho kilicho na uwezo wa kucheka nafsi za watu wengine. Mwandishi amekihuisha na kukifanya kina uwezo wa kucheka nafsi za wengine kama alivyo binaadamu.

Tash-hisi nyengine zilizotumika katika Tamthilia hii ni kufa kwa mawazo (uk. 82), ulimwengu umetufunza (uk. 62, 63).

Kipengele hiki hakikujitokeza katika tamthilia ya Mbaya Wetu. Inawezekana kuwa tafauti hii imekuja kutokama na upekee wa mbinu za kisanaa alizonazo mwandishi na dhamira alizotaka kuziwasilisha. Pia yawezekana kuwa ni tafauti za umahiri wa lugha walionao watunzi hawa kutokana na tafauti za kimazingira. Mohamed anaonekana kuwa na umahiri mkubwa zaidi wa lugha ya Kiswahili anayoimudu kufinyangika zaidi kifasihi.

Usambamba: Wamitila (2003) ameleza kuwa, hii ni mbinu ambapo msanii anayarudia maneno fulani au maana fulani kwa muundo mwingine tofauti. Urudiaji huu unaweza kuwa katika viwango tofauti kama vya vipashio vya kisintaksia, virai, vishazi au sentensi. Vipashio vya kisintaksia vinaweza kupangwa kwa namna inayowezekana kuleta maana sawa. Matumizi ya usambamba yamejitokeza katika Amezidi na hayakutumika katika Mbaya Wetu. Kwa mfano, katika (uk. 28) Zidi anasema,

“Nyamaza . . . nyamaza . . . hajatambua, hajajua tu, hujabaini utajiri wetu na raha zetu akibaini tarudi kimbelebele au kinyumenyume au hata kiubavubavu; ngoja tu!”(uk 28).

Lakini pia usambamba umejitokeza tena katika nyimbo (uk. 29):

“Tunaimba wimbo huu

Mwimbo wa fahari na makuu

Tunaimba kuisifu rangi hii ya fuu

Rangi ya mkaa

Rangi ya mpingo . . .” (uk 29)

Mwandishi katika dondoo hii anazungumzia kuhusu bara la Afrika na kulisifu kwa ufahari. Kusifu rangi ya fuu ambazo zikiiva na kuwa tayari kuliwa zinakuwa na rangi nyeusi. Ametumia pia rangi ya mkaa ambayo pia ni nyeusi; ametumia rangi ya mpingo mti ambao pia una rangi nyeusi kwa kumaaanisha bara la Afrika linalokaliwa na Waafrika wengi wao wakiwa ni wale weusi. Amechagua msamiati fuu, mkaa, na mpingo kwa lengo mahasusi la kuudhihirisha Uafrika katika Bara la Afrika. Pia, mwandishi anaonesha kuwa, weusi huo, ni rangi yenye kiza kwa maana ya ujinga na uovu unaofanywa na waafrika wenyewe hali inayoligubika bara hili la Afrikana na kuliweka nyuma kiuchumi na kisiasa.

Vilelevile, usambamba unaonekana katika Amezidi (uk. 34) wakati mwalimu alipokuwa anamuuliza maswali mwanafunzi kuhusu nyambizi na mwanafunzi kushindwa kujibu kwa usahihi. Mwanafunzi anasema,

“Nyambizi ni nyama, dudu, nyangarika, dubwana, dude, linalozamia au linalopiga kachombwe na kuogelea chini kwa chini linalosonga katika vina mbalimbali vya maji-bahari” (uk. 34).

Misamiati yote hii aliyoitumia mwandishi inaonekana inafanana kidhima. Misamiati hii nyama , dudu, nyangarika dubwana, dude, hujenga taswira kama kitu kisicho cha kawaida, kinachoeleweka bayana kutokana na sifa zake bainifu. Mohamed ametumia usambamba huo kwa lengo la kuonesha namna (walimu) viongozi wetu wa Kiafrika walivyo na ubabaifu, wasivyofahamu na wanavyoshindwa kuyaelewa mambo muhimu kwa wanaowaongoza pamoja na kuyatatua matatizo yanayozikabili jamii zao. Usambamba unaonekana pia katika uk. 62, 63, 65. Kwa upande wa tamthilia ya Mbaya Wetu mwandishi hakutumia usambamba.

Tafauti hii inatokama na umahiri wa lugha. Matumizi ya usambamba yanahitaji umahiri mkubwa wa lugha kwa mwandishi. Mwandishi ambaye anaandika kwa kutumia lugha ya pili yawezekana asiweze kutumia mbinu hii ya uandishi; kwani ni mbinu inayohitaji kuwa na uelewa ama utajiri mkubwa wa misamiati ya lugha

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

anayoiandikia. Tunapowanagalia waandishi hawa wawili, mmoja ni mzawa wa Kiswahili na mwingine Kiswahili ni lugha yake ya pili.

Ritifaa: Hii ni mbinu ya kumsemesha mtu au kitu kisichokuwapo. Mbinu hii imejitokeza katika Amezidi na haipatikani katika Mbaya Wetu. Mbinu hii imetumika katika (uk 85):

“Ame: Majirani

Sauti: Kuzimu ...

Ame: Nahapa wapi?

Sauti: Kuzimu

Ame: Hapana, hapa Afrika . . . hii ni Afrika.

Sauti: Kuzimu . . . kuzimu . . . KU- ZI- MU . . .”

Mwandishi ametumia mbinu hii kutilia nguvu kile alichozungumza na hivyo maudhui ya mwandishi yamemsukuma zaidi kutumia mbinu hii. Kwa mafano, katika tamthilia ya Amezidi mwandishi anatilia nguvu udhaifu na uoza unaofanyika katika nchi mbalimbali zilizo katika bara la Afrika.

Sitiari: Hii ni tamahali inayolinganisha vitu au watu bila kutumia viunganishi-linganishi. Katika tamathali hii vitu na watu hulinganishwa na vitu na watu wengine kama kwamba vitu na watu hao ni sawa kabisa. Katika tamthilia ya Mbaya Wetu, sitiari zimetumika kwa kiasi kidogo ukilinganisha na tamthilia ya Amezidi. Katika Mbaya Wetu sitiari zinaonekana katika uk 45 na 65. Tabia ni ngozi (uk 47), mwanangu Matari mboni ya jicho langu, ua la moyo wangu” (uk 65).

Kwa upande wa tamthilia ya Amezidi, sitiari zimetumika kwa kiasi kikuwa zaidi ambapo kazi nzima imjengwa kisitiari na kubeba mafumbo mengi. Ili kuifahamu tamthilia hiyo ni lazima uzipasue sitari hizo kwa umakini. Bila hivyo msomaji hatofahamu mwandishi anazungumzia nini. Sitiari zimetumika uk 5, 23, 29, 65, 66, 72, 86. Kwa mfano, Zidi anamuuliza Mari,

Zidi: Unatoka wapi Mari?

Mari: Mbali

Zidi: mali wapi?

Mari: Kutoka katika Giza na vumbi la kuwezwa na kumezwa...
(uk 65).

Katika dondoo hii mwandishi anamithilisha ‘giza na vumbi’ na ujinga wa vijana wa kuiga utamadumi usiona faida kwao, uliotanda katika fikra zao.

Ingawa waandishi wote wametumia sitiari, kuna tafauti iliyojitokeza kati yao. Katika tamthilia ya Amezidi sitiari zimetumika nyingi zaidi. Hali hii inatokana na sababu tafauti. Kwanza Amezidi ni tamthilia ya Usasabaadaye kinyume na Mbaya Wetu ambayo ni ya uhalisia. Kwa kawaida kazi za usasabaadaye huwa na sitiari nyingi zaidi kuliko zile za Uhalisia.

Pili, dhamira zilizotumika katika tamthilia hizi zinatafautiana kidogo. Kawaida kazi zinazozungumzia dhamira nzito za kisiasa mara nyingi hutumia sitiari zaidi kuliko zinazozungumzia dhamira za jamii. Pia kazi hizi mara nyingi zinakuwa na lugha nzito za kifalsafa ambazo zinahitaji tafakuri za hali ya juu ukilinganisha na kazi za uhalisia. Hivyo matumizi ya sitiari yanamfanya msomaji kutafakari kwa undani ili kufahamu kazi hiyo. Kwa mfano katika tamthilia ya Amezidi tunapata sitiari kama, muhogo uliovunda, kama inavyojitokeza katika dondoo hapo chini.

Zidi: Aha . . . unasema mhogo uliovunda?

Ame: Mhogo uliovunda? Nani kataja muhogo uliovunda au una njaa?

Zidi: Mhogo uliovunda enh!

Ame: mhogo tekea lini kuvunda?

Zidi: Ah, (anafanya kukumbuka kitu) kweli mhogo hauvundi.

Huambatwa na ukungu tu ambao ukiukwangurakwangura basi utalika; lakini hata mwanadamu huambatwa na ukungu na mara nyingi ukimkwangura kwangura hasafiki . . . (uk 5).

Ukungu uliomuambata mwanadamu ni sitiari, inayofananishwa na fadhaa wanazojitia viongozi katika kutekeleza ahadi walizowapa raia wao. Ukungu huu

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

usiokwangurika ni kutokubadilika kwa viongozi. Daima anapokuwa juu ya wengine huendelea kufuata tabia zilezile kama za watawala wakongwe - kama walivyokuwa wakoloni, walikuwa wakiishi maisha ya juu na kifaghari na kuwakandamiza wengine. Maisha kama hayo ndiyo wanayoishi viongozi wa kisiasa wa leo Afrika. Kutoa amri kali na hasa kwa lengo la kuwalinda wao na rasilimali walizohodhi, kutembelea magari ya kifaghari na kujilimbikizia mali nyingi lakini raia wengi wanateseka na hali ngumu za maisha na huduma duni za kijamii, kuishi katika nyumba zisizoridhisha na hata wengine kufa kwa njaa na maradhi.

Mfano mwengine wa sitiari ni mti msowera ulioota katika moyo wa Mari na Zidi.

Mari: Mti . . .

Zidi: umefanyaje?

Mari: Umeota – umenawiri moyoni mwako!

Zidi: Mti . . . mti . . . umeota . . . umeota . . . moyoni mwangu. . .
(Hofu na macho katoa)

Mari: Usiogope . .

Zidi: kwa nini?

Mari: kwa sababu mti wenywe mjinga

Zidi: Mjinga?

Ame: Mjinga enh, mjinga mwangamizi!

Mwandishi anaonesha namna vijana alivyotekwa akili zao na tamaduni za kigeni. Hasa za Kimagharibi kiasi kwamba wanafikia hatua ya kudharau maumbile waliyopewa na Mungu na kutoridhika nayo. Kutokana na athari hizo, huamua kujibadilisha rangi zao na nywele ili wafanane na wenye utamaduni uliowateka licha ya kuwa wamepewa rangi nzuri isiyoigika, nywele nzuri zinazowapendeza kulingana na maumbe yao.

Maswali ya balagha (rhetorical questions): Hii ni mbinu ambayo hutumia maswali ya kawaida lakini hayahitaji majibu, kwani majibu yake huwa yanafahamika. Mbinu hii imetumika katika sehemu mbalimbali katika Amezidina lakini haikutumika katika

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

Mbaya Wetu. Kwa mfano, “Tokea lini pono kuamka?”(uk. 4); “Kazi ya nini?” (uk 8); “Kwani kucha huna?” (uk. 11); Kuvumbua kwa nini?” (uk 37) na kadhalika.

Tafauti hizi za matumizi ya kibalgha zinatokana zaidi na uchaguzi wa zana ya kisanaa kwa mwandishi mwenyewe. Mwandishi ametumia maswali ya kibalgha ili kuleta uzingativu kwa hadhira yake na kuisistiza dhamira aliyotoa. Lengo ni kuitaka hadhira ione matatizo iliyonayo ndani ya bara lao la Afrika.

Mafumbo: ni usemi au msemu unaotumika ili kusitiri maana fulani inayokusudiwa. Mara nyingi maneno hayo huwa na busara au falsafa fulani ndani yake. Mbinu hii imetumika katika tamthilia zote mbili ingawa kuna tafauti kidogo. Katika Amezidi mafumbo yaliyotumika ni ya kiwango cha juu zaidi ukilinganisha na kwenye Mbaya Wetu. Hali hii inatokana na uzito wa maudhui iliyojadiliwa katika tamthilia husika.

Tukianza na Amezidi mwandishi ametumia mafumbo katika kianzio (uk 1-3) katika ‘Wimbo wa Mzee’. Kwa mfano, katika wimbo huu mzee anautuma wakati upeleke salamu kuzimu kuwa naye yuko njiani anakwenda. Pia anaendelea kueleza jinsi alivyosumbuka kwa kubeba mzigo mzito wa dunia akidhani amepewa na Mungu kumbe ni mzigo aliobebeshwa na wanadamu wenzake. Maelezo yote katika nyimbo hiyo ni mafumbo yanayoonesha matumaini yake, maelezo ya wote aliowashuku na matumizi ya nyakati, jana, leo na kesho ni mafumbo.

Pia, ametumia mafumbo kama muhogo, kulala na kuamka, kisu, raha ya kifo na mauti, kulala kufa au kufa kulala, kucheka na kulia, mti msowera ghaibuni, mti mjinga mwangamizi, uvundo, safari na kiza, mapenzi au mlambatano, ndani ya tumbo la bara la Afrika n.k. Mwandishi ametumia mafumbo mengi ambayo yanahitaji tafakuri kubwa wakati msomaji anapoisoma tamthilia hii. Mafumbo hayo anaweza kuyafumbua kulingana na miktadha ya matumizi.

Katika Mbaya Wetu mafumbo yaliyotumika zaidi yapo katika muundo wa kimethali kama zilizooneshwa juu. Pia katika (uk 70)“ ...simba wameachiliwa tena katika msitu wa kondoo?” Katika tamthilia hii, mwandishi anaonekana kujikita zaidi katika maudhui inayohusu maadili, malezi na mambo mengine ya kijamii. Hivyo ametumia mafumbo ya methali zaidi kutokana na dhima kuu za methali hizo, na dhamira alizozielekeza katika tamthilia yake.

Vitendawili: Tafauti pia inajitokeza katika matumizi ya vitendawili. Katika tamthilia ya Mbaya Wetu havikutumika, lakini kwa upande wa Amezidi mwandishi

ametumia vitendawili. Mfano mzuri ni Kitendawili kinachoonekana katika mazungumzo kati ya Bosi na Msaidizi wake wakati walipokuwa wanapitia orodha ya vitu vinavyotaka kununuliwa kwa matumizi ya ofisi. Bosi na msaidizi wake wanategeana kitendawili “orodha ndefu, orodha nono” jibu lake “Mambo mpango!” (uk 43 47). Mwandishi ametumia kitendawili hiki kwa lengo la kuonesha mbinu za ubadhirifu zinazofanywa na wafanyakazi katika ofisi za umma. Namna mabosi na wasaidizi wao wanavyotumia fursa hiyo kupanga njama za kuhujumu fedha na uchumi wa uma kwa kutumia nafasi walizowekwa. Mwandishi ametumia mbinu hii kuipamba kazi yake ili kudhihirisha ufundi wa lugha ya kifasihi aliyonayo na kuifanya kazi iwe ya kuvutia..

Ukinzani: Tafauti nyengine ni matumizi ya ukinzani. Hii ni mbinu anayotumia mwandishi inayotoa maelezo kuhusu dhana mbili zenye maana zilizokinyume kabisa. Mbinu hii imetumika katika Amezidi na kuifanya ijitafta na Mbaya Wetu. Mfano huu wa kukinzana kwa maneno haukutumika katika Mbaya Wetu. Hali hii inatokana na umahiri wa lugha wa mwandishi, unaomwezesha kucheza na lugha kwa umakini mkubwa. Kwa mfano, katika Amezidi imetumika sehemu tafauti kama,

Mzee anayeelekea kufa na mtoto ambaye hajazaliwa (uk 90), ‘naitazamia kesho katika mauti’ (uk 3), ‘msiba na kichekesho pia . . . kucheka uchungu’ (uk 24), ‘suala jibu’ na ‘jibu suala’ (uk 32), ‘kusema kunyamaa’ na ‘kunyamaa kusema’ (uk 37), ‘wamelala- kufa’ na wamekufa- lala’ (uk 41), ‘nilicheka, nikalia’ (uk 44), ‘tumacho tumelala’ au ‘tumelala tumacho’ (uk 68), ‘lala baba lala au amka . . .amka milele’ (uk 73), ‘mwanzo unaoanza mwisho’ (uk 86) n.k.

Mwandishi ametumia maelezo hayo yanayoleta hali ya kutatanisha kwa lengo la kujenga umakini na tafakuru kwa msomaji ili aweze kuelewa maana na tafauti ya dhana hizo ili kumwezesha kupata ujumbe uliokusudiwa uikie hadhira.

Matumizi ya kejeli / kinaya: Kipengele hiki kinaonesha kufanana kwani waandishi wote wamekitumia. Kejeli/ Kinaya ni matumizi ya lugha ambapo mwandishi hueleza jambo lililo kinyume na matarajio ya hadhira yake au jambo ambalo tayari hadhira inalifahamu kuwa ni kinyume cha ukweli ulivyo. Katika Amezidi kejeli zifuatazo zimetumika:

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

‘Raha ya kifo’ na ‘Hapana Kifo cha raha’ (uk 41), ‘Tokea lini pono akaamka’ (uk 4), ‘Suruali au ghuba’ (uk 5), ‘Na kwa nini mtu apende kazi? Mungu yupo na ardhi ipo . . . na ardhi yenyewe bikra... (uk 7), ‘Umeshapeleka maombi ya msaada huko umoja wa mataifa? Au kuomba ruzuku nchi za Magharibi yaani EC (uk 9), Aaaa shida yote ya nini bwana. Kabla kibiriti hakijavumbuliwa wazee wetu walikuwa wakifanya nini?’ (uk 12) n.k.

Kejeli hizo hapo juu ni tashtiti zinazokosoa bila kukasirisha na zinazoonesha uoza unaofanywa barani Afrika. Mwandishi ametumia kejeli hizo kutoa shutuma dhidi ya uvivu na ombaomba, inayowakatisha tamaa wanyonge kwa kuona kuwa, maisha haya ni majanga tu, na hayana tija kwao, hadi kufurahia kifo ambacho kwa kweli si kitu cha raha.

Kwa upande wa Mbaya Wetu mwandishia metumia kejeli kama vile: “Hewalla ndugu imamu. “... Bila shaka kwema tu . . . tena nyumba ya Bwana Temba njema tangu hapo ... Nyumba ya Amani na muamana na itifaki. Haijui mawimbi yanayosukasuka watu wengine hapa kijijini.” (uk 39).

Ingawa waandishi hawa wote wametumia kejeli lakini kumejitokeza tafauti kidogo. Kejeli zilizotumika katika Amezidi zinaonekana kuwa ni za kimafulumbi zaidi, ukilinganisha na zilizomo katika Mbaya Wetu. Tafauti hii inatokana na dhamira alizojadili mwandishi hasa ukizingatia kuwa tamthilia ya Amezidi ni aina ya Tamthilia ya Ubwege. Katika tamthilia za aina hii kejeli hutumika kwa kiasi kikubwa kuliko katika tamthilia za aina nyengine.

Ushikamano: Ni matumizi ya vijenzi maalum vinavyotumika kuunganisha matini. Kwa mujibu wa Halliday na Hassan (1976) nukuu kutoka kwa Ziada H. A. katika tasnifu yake ya Uzamili (Haijchapishwa) anaeleza kuwa,

Ushikamano ni uhusiano wa kimaana uliomo katika matini na ambao huitambulisha matini...hii ni rasilimali ya uundaji wa matini, inayoonesha kiwango cha maana ambayo ni maalumu kwa kile kinachozungumzwa na kuandikwa katika mazingira yake ya kimaana... wameeleza kuwa ushikamano ni dhana ya kisemantiki ambayo huonesha uhusiano wa kimaana ambao umo katika matini na ambayo huifanya matini kuwa matini... ushikamano ni mkusanyiko wa rasilimali za kisarufi, ambazo zimo katika kila lugha

(kama sehemu ya mfumo wa kiisimu ambao huunda maana katika matini), kwa kuunganisha sehemu moja ya matini na nyengine. Kwa hiyo ushikamano katika lugha, ndio nyenzo kuu ya kuleta maana katika matini, ili isikike au isomeke na kufahamika kile kilichosemwa au kuandikwa.

Wataalamu hawa wameuonesha ushikamano katika makundi mawili ambayo ni Ushikamano wa kisarufi /sentensi (Grammatical Cohesion) na ushikamano wa maneno (Lexical Cohesion). Vile vile Wamitila (2008) anaeleza kuwa, katika kushikamanisha na sentensi hizi, kuna vijenzi maalumu vya ushikamano (cohesive tie au cohesive devices) vinavyotumika. Vijenzi vya ushikamano, (cohesive tie) ni maneno au sehemu ya neno katika matini, ambayo huunganisha sehemu tofauti za sentensi na kufanya / kutengeneza matini iliyokusudiwa (Wamitila 2008).

Ushikamano umetumika kwa maandishi wote wawili. Kwa mfano, katika Amezidi (uk 56) muunganiko unajitokeza kupitia sentensi zifuatazo. “Ah! Kweli ... hata nilisahau kwamba wewe ndugu yangu...Na ndugu hawalani wala hawaumani...Badala yake? Huhifadhiana ... hupendana ... husaidina; ukila wewe na ndugu yako mpe; ...”(uk56). Tunaona namna mwandishi alivyotumia viambishi vya ukanushi ‘ha’ na nafsi ya tatu wingi ‘wa’ pamoja na viambishi vya hali ‘hu’kuunda aya iliyoshikamana vizuri na kuleta maana iliyokamilika.

Kwa upande wa Mbaya Wetu (uk. 27) Lila anasema, “...Yamkini wachinjaji walimchinja usiku wakasomba nyama zote wakazifungia kwenye bucha. Lakini kichwa wakakisahau machinjioni.” Mwandishi ameunganisha sentensi katika aya hizi kwa kutumia kiambishi cha nafsi ya tatu wingi kuijenga aya iliyoshikamana na kuleta maana nzuri.

Mwingilianomatini: Mwingiliano matini ni dhana inayorejelea uhusiano wowote unaoweza kuonekana katika matini moja na nyengine au matini zaidi ya moja. Uhusiano huo unaweza kujitokeza katika kipengele kimoja au vipengele mbalimbali, fani, maudhui au vyote kwa pamoja (Jilala 2016). Allen (2000) anafasili mwingilianomatini kwa kusema ni dhana yenye maana ya uhusiano, muunganiko na kutegemeana na utamaduni wa kisasa katika enzi hizi za kiusasabaadaye ambapo wanamwingilianomatini huona kuwa si rahisi kuzungumzia uasili au

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

upeekee wa kazi ya sanaa, kwani kila kazi ya sanaa inatokana na kazi tangulizi. Kristeva (1980: 66) anasema kuwa matini yoyote imeundwa kwa mkusanyiko wa nukuu na ni ufyonzaji na ubadilikaji wa matini nyengine.

Hivyo hali hii pia inathibitika katika kazi hizi mbili. Katika tamthilia za Amezidi na Mbaya Wetu waandishi Mohamed na Walibora wanaonekana kutumia mbinu hii ya mwingilianomatini. Tukianza na tamthilia ya Mbaya Wetu, mwandishi ametumia sentensi kama vile,

1. Kitumbua changu msinitilie mchanga, (uk 65).
2. Kumbuka kisa cha mwana mpotevu katika maandiko, (uk 66).
3. Gharika ya Nuhu, (uk 72).

Katika mifano iliyopo hapo juu, mfano na. 1 unahusiana na usemi maarufu katika jamii za waswahili lakini pia unahusiana na kazi ya fasihi ya mwandishi Said Ahmed Mohamed yenye anuani Kitumbua Kimeingia Mchanga. Msemo huu hutumika kuonesha hali ya kukitia kitu kasoro au jambo fulani na kuliharibu au kulifanya lionekane limeharibika. Katika mfano 2 na 3, ni sentensi zinahusiana na kauli za simulizi za maandiko matakatifu ya kidini. Kwa mfano, Kisa cha mwanampotevu kinapatikana katika Biblia, Luka:15:11-30. Na gharika ya Nuhu ni kisa kinachoelezwa katika Kur-ani Tukufu na hata katika Bibilia.

Mwandishi ametumia matini hizo za mwanzo kukamilisha matini yake kutokana na lengo alilokusudia kulionesha katika kazi yake . Enani (2005) anasisitiza kuwa matini mbili au zaidi huwa na uhusiano katika kiwango ambacho kinaathiri namna ya usomaji mpya. Hapa tunaona namna matini hizo zinavyoathiri usomaji mpya unaomfanya msomaji kurejelea akilini mwake kisa cha nyuma na baadaye kuunganisha na kisa kilichomo katika kazi mpya anayoisoma.

Kwa upande wa tamthilia ya Amezidi, pia kumejitokeza mwingilianomatini kama inavyothibitishwa katika sehemu mbalimbali. Kwa mfano, mhusika Ame anaeleza:

“...Kwa nini mtu apende kazi. Mungu yupo na ardhi ipo ...na ardhi yenywe bikira ... ikidondoka tu mbegu imeshaota! Ikidondoka kambu ya mgomba kesho utakula ndizi na hapa mwaka mzima ardhi inakubali tu, haichoki . . . wewe kulala tu na kulala!” (uk. 7).

ULINGANISHI WA TAMTHILIA ZA KISWAHILI: Mifano Tamthilia ya Mbaya Wetu na Amezid

Saade Said Mbarouk

Pia mwingilianomatini unaonekana katika (uk 12). Mhusika Ame na Zidi wanapojadiliana.

Ame: Aaa, shida yote ya nini bwana? Kabla kibiriti hakijavumbuliwa wazee wetu walikuwa wakifanya nini?”

Zidi: Wakipekecha moto.”

Tunaona mifano hiyo imeathiriwa na kuingiliana na masimulizi ya kale ambayo yamesaidia kujenga matini hii.

Vilevile, katika tamthilia hii tunapata mwingilianomatini wa kiutamaduni. Katika jamii mwanamke anahimizwa sana kuhusu usafi hivyo kauli kama hizi hujitokeza sana hasa katika nyimbo za taarab za kisasa/mipasho inayozungumzia usafi wa mwanamke. Katika tamthilia hii mwandishi amemtumia mhusika Mari kuionesha hali hiyo kama inavyoonekana hapo chini.

Mari: Kwamba mtu, ah – mwanamke ni kivazi, mwanamke ni kujipodoa, mwanamke ni kujikwatua na kuupura” (uk. 64).

Pia katika (uk 85), wakati Ame alikuwa akiisogelea hadhira na kusema,

“Ilikuwa ndoto enh!Ndoto au ukweli unaonata ... ukweli unaouma? Ni kama kuota ndoto ukaelekea kiza . . . Ni kama kugeuka nyuma na kuelekea mbele iwapo kote kuna kiza kutazama Pepo ya Aden au Bustani inayonin’ginia ya Babilon au kitalu cha Adam na Hawa . . . mbali kule yanakotoka . . . na mbali kule tunakokwenda...” (uk. 85- 86.)

Katika sehemu hii tunaona namna matini hii ilivyoathiriwa na matini za kale za kihistoria zinazoeleza uzuri wa mazingira. Kwa mfano, kitalu cha Adam na Hawa na Na pepo ya Aden, tunapata simulizi hizi kutoka katika vitabu vitakatifu kama Qur-an na katika Biblia.

Hivyo kupitia sehemu hii tunaona namna waandishi hawa wawili walivyofanana. Wote wamejenga matini zao kutokana na athari za baadhi ya matini zilizotangulia. Msomaji anapoisoma moja kwa moja anaweza kuhusisha uzoefu alionao katika maisha, kupitia mambo aliyoyaona au kuyasikia yeye mwenyewe au aliyoyasoma sehemu na kuhusisha na kazi hiyo mpya.

Kauli hii inaunga mkono kauli ya Bakhtim (1895;1975) kupitia nadharia yake ya Usemezano au daiolojia kwa kusema kuwa kila tamko ni athari ya matamko mengine yaliyotangulia au yatakayofuata; matamko yaliyotangulia huchochea tamko au matamko ya baadaye. (Wamitila 2003:5; Kyarenda, 2014:56) nukuu kutoka Jilaa (2016).

Hitimisho

Makala hii imelinganisha tamthilia mbili za Amezidi na Said Ahmed Mohamed kutoka Tanzania na Mbaya Wetu na Ken Walibora kutoka Kenya. Ulinganishi huu umejikita katika vipengele vya fani ambapo vipengele vilivyoshughulikiwa ni pamoja na muundo. Katika kipengele hiki makala imeangalia ploti, wahusika na mandhari. Mandhari imefafanuliwa kupitia miktadha mbalimbali iliyotumika katika riwaya zote mbili. Kipengele chengine kilichojadiliwa ni mtindo ambapo vipengele vilivyochunguzwa ni matumizi ya lugha. Katika kipengele hiki, ulinganishi umefanywa katika taswira na ishara, tamathali za semi pamoja na mbinu nyengine za kisanaa, kama, methali mwingilianomatini, ushikmano, n.k. Kazi zilizolinganishwa zimeonekana kutafautiana kutokana na mkabala uliotumika pamoja na dhamira zilizotolewa na waandishi.

MAREJELEO

- Ali, Z. H (2017) "Ushikamano wa Sentensi Katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganishi wa Nyota ya Rehema a Utengano." Tasnifu ya Shahada ya uzamili. Chuo Kikuu cha taifa cha Zanzibar. (hajachapishwa).
- Bassnett, S (1993/1995). Comparative Literature: A Critical Introduction. Oxford UK & Cambridge: USA: Blackwell.
- Boldor, A. (2003) "Perspectives on Comparative literature" https://digitalcommons.lsu.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=4866&content=gradschool_thesis_10/6/2018
- Catherinebrown.org/wordpress/wp-content/uploads/2014/03/what-is_Comparative_Literature_pdf. 23/10/2016
- Hutchen, L. (1996) "Comparative Literature's Anxiogenic State" Canadian Review of Comparative Literature. (35-41)
- Halliday, M.A.K. na Hassan, R. (1990): Language, Context and Text: Aspect of Language in a Social –Semiotic Perspective. Oxford University Press. United Kingdom.
- Halliday, M.A.K. na Hassan, R. (1976). Cohesion In English. Longman Inc Publishers. New York.
- Halliday, M. A. K. (1985). An Introduction to Functional Grammar. London.
- Jilala, H. (2016). Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi. Daud Publishing Company: Dar es Salaam.
- Kiango, S. D. (1979), "Tamthilia za Kiswahili na Mabadiliko ya Dhamira" Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Hajachapishwa).
- Madumulla, J. S. (2009). Riwaya ya Kiswahili: Historia, Nadharia na Misingi Uchambuzi. Dae es Salaam: Mture Educational apublishers.
- Manyamacharles.blogspot.com/2014/06/Tafsiri na fasihi linganishi- ya.html. 21/11/2016.
- Martin, E. (1996) The Framing of Comparative Literature, or Is Comparative Literature What Culture is to studies? The comparatist(25- 40).
- Mohamed, S. (1995). Amezidi. English Press Ltd: Nairobi.
- Nauta, D. Jr. (1972) The Meaning of Information. The Haque: Mouton:
- Njogu, K. na Chimera (2011). Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomokenyata Foundation.
- Ponera, A. (2014) Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi. Karljamer Print Technology: Dar es Salaam.

- Steiner, G. (1995) "What is Comcarative Literature?" Oxford: Clarendon Pres
- Walibora, K. (2014). Mbaya Wetu. Autolitho Ltd: Nairobi.
- Wamitila, K.W. (2003), Kamusi ya Fasihi: Istilahi, na Nadharia, Focus Publication Limited, Nairobi.
- Wafula, R. M. (2003) Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002) Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake. Nairobi. Phonex Publishers.
- Weisstein, U. (1973) Comparative Literature and and Literary Theory. Bloomington& and London: In-diana U. P.
- Wellek, R. &Warren, A. (1996) Theory of Literature. New York: Braceand Company.
- Wellek, R (1988) "The Crisis of Comparative Literature" Concept of Criticism. Ed. Stephen G. Nichols, Jr. New Haven: Yale UP, 282- 95.
- The 7 or Seven Days of Creation Undated Past, Genesis.<https://bibleview.org>
- Luke 15:11-32 Niv – The Parable of the lost son: Gesuss: Bible gateway.15/5/2018
- <https://bible gateway.com> 12/5/2018
- [https://www.rsearchgate.net/publication/236660739-Comparatib Literature_and the Question_of_Theory](https://www.rsearchgate.net/publication/236660739-Comparatib_Literature_and_the_Question_of_Theory).18/10/2016.
- [https://en.wikipdia.org/wiki/Comparative Literature](https://en.wikipdia.org/wiki/Comparative_Literature). 18/10/2016.
- <https://wwwprivatewriting.com/compare-contrast-essay>. 5/11/2016.